**BARAZA LA TAIFA LA ELIMU YA UFUNDI NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI (NACTVET)**

**TAARIFA KWA UMMA**

# MATOKEO YA UCHAGUZI WA UDAHILI KUPITIA MFUMO WA UDAHILI WA PAMOJA (CAS) KWA KOZI ZA AFYA NA SAYANSI SHIRIKISHI KWA MWAKA WA MASOMO 2025/2026 - AWAMU YA NNE

Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET) linautangazia umma matokeo ya uchaguzi wa awamu ya **nne** (4) kwa waombaji wa programu za **Afya na Sayansi Shirikishi** kwa mwaka wa masomo **2025/2026**.

Baraza liliratibu udahili wa wanafunzi awamu ya nne katika kozi mbalimbali za Afya na Sayansi Shirikishi kupitia Mfumo wa Udahili wa Pamoja (CAS) kwa mwaka wa masomo 2025/2026. Jumla ya waombaji **7,024** walikamilisha maombi yao kwa kuchagua vyuo na programu walizozipenda. Kati yao, jumla ya waombaji **6,304** walitimiza sifa za kujiunga na programu walizoomba na waombaji **720** hawakukidhi sifa za programu walizoomba.

Jumla ya waombaji **2,439** wamechaguliwa kujiunga kwenye vyuo vinavyotoa programu mbalimbali za Afya na Sayansi Shirikishi ambapo wanawake ni **1,256 (51.5%)** na wanaume ni **1,183 (48.5%).** Waombaji **76** walichaguliwa kwenye vyuo vya serikali na waombaji **2,363** katika vyuo visivyo vya serikali.

Waombaji wote wanaweza kuangalia matokeo ya uchaguzi kupitia tovuti ya Baraza (www.nactvet.go.tz) kwa kubonyeza ***CAS Selection 2025*** ili kupata taarifa zaidi.

Kwa muktadha huo, Baraza linautaarifu umma kwamba vyuo vitafunguliwa rasmi **tarehe 3 Novemba, 2025** kwa waombaji wote waliochaguliwa. Sambamba na hilo, Baraza linasisitiza kuwa kila mwanafunzi ahakikishe anasajiliwa kwenye mfumo wa Baraza kuanzia tarehe **3 Novemba hadi 12 Desemba 2025.**

**IMETOLEWA NA:**
**OFISI YA KATIBU MTENDAJI**
**BARAZA LA TAIFA LA ELIMU YA UFUNDI NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI (NACTVET)**
**21/10/2025**